
# SAUTI YA TSC

TOLEO NA.3 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) MEI 2021

# MWL. NKWAMA AAPISHWA KUWA KATIBU TSC




*Mwl. Paulina Nkwama akila kiapo mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kushika wadhifa wa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Aprili 6, 2021 Ikulu jijini Dar es Salaam.*

**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz**

*Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania* *tumeyautumishiwawalimutanzania*

# TSC TUADHIMISHE MEI MOSI HII TUKIONGOZWA NA KAULIMBIU YA 'KAZI IENDELEE'

Leo familia ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tunaungana na wafanyakazi wenzetu wa kada mbalimbali duniani kote kuadhimisha sikukuu ya wafanyakazi, maarufu kama 'Mei Mosi'

Ziko namna nyingi za kuadhimisha sikukuu hii zikiwemo sherehe na maandamano. Sisi familia ya TSC, pamoja na kusherehekea sikukuu hii adhimu, tunawiwa kuiadhimisha huku tukiongozwa na kaulimbiu ya Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ya '….Kazi Iendelee'

Kazi Iendelee kwa kuendelea kusimamia maadili mema kwa walimu wa sekta ya umma. Tuendelee kuhakikisha walimu tunaowasimamia wanawalea watoto wanaopita katika mikono yao kimwili, kiakili, kiroho na kijamii.

Tuendelee kuwaongoza walimu katika kuhakikisha hawageuki 'miiba' kwa wanafunzi kwa kuenenda kinyume na maadili yao na kuwatendea yasiyopaswa kutendwa ikiwemo kujihusisha nao kimapenzi na kuwa watoro kwa kufundisha vipindi vichache tofauti na wanavyotakiwa kufundisha.

Lakini pia, Kazi Iendelee kwa kuhakikisha tunaendelea kushughulikia matatizo ya walimu yaliyoainishwa katika majukumu yetu, ikiwemo kuhakikisha haki inatendeka pale wanapotuhumiwa kwa makosa mbalimbali. Kamwe tusiwe sehemu ya kuwanyanyasa au kuwaonea walimu kwa namna yoyote.

Tukumbuke kuwa TSC ilianzishwa kwa malengo ya kuongeza ufanisi katika kuwahudumia walimu ambao ni kundi kubwa linalochukua asilimia zaidi ya 50 ya watumishi wa umma. Hivyo, tunawajibika kuhakikisha malengo husika yanatekelezwa kikamilifu.

Tunawatakia nyote maadhimisho mema ya sikukuu ya wafanyakazi duniani. TSC….**Kazi Iendelee!**

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
**Paulina Nkwama**

**Wajumbe**
Moses Chitama
Christina Hape
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya

**Mhariri Mkuu**
Veronica Simba

**Mhariri Msaidizi**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

## KATUNI

MAADHIMISHO YA SIKU YA WAFANYAKAZI DUNIANI 2021




**Wasiliana nasi kwa Simu:** 0739-669610 & 0735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***

*Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania* *tumeyautumishiwawalimutanzania*

# MWL. NKWAMA AAPISHWA KUWA KATIBU TSC



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akitia saini hati ya kiapo ya Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, Aprili 6, 2021 Ikulu jijini Dar es Salaam.*

**Na Veronica Simba**

Katibu mpya wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, aliyeteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan hivi karibuni, ameapishwa rasmi kushika madaraka hayo.

Mwl. Nkwama aliapishwa na Rais Samia, Aprili 6 mwaka huu katika hafla iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam, sambamba na wateule wenzake mbalimbali katika nafasi za Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Wakuu wa Taasisi.

Akizungumza mara baada ya kuwaapisha Viongozi hao, Rais Samia aliwataka kuhakikisha wanasimamia majukumu na kutekeleza wajibu wao ipasavyo kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020/25.

Katika Sekta ya Elimu ambayo TSC inahusika nayo, Rais Samia alielekeza kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya elimu, ikiwemo shule 26 za sekondari za wasichana pamoja na kujaza nafasi 6,000 zilizoachwa wazi na walimu waliostaafu.

Mwl. Nkwama aliteuliwa na Mheshimiwa Rais Machi 29, 2021 ambapo aliripoti ofisini na kuanza kazi mara moja hapo Aprili 1, mwaka huu, akichukua nafasi ya Winfrida Rutaindurwa ambaye amemaliza muda wake.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, akisaini kiapo alichoapa mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kushika wadhifa huo, Aprili 6, 2021 Ikulu jijini Dar es Salaam.*

# MAAFISA ELIMU KATA WAASWA KUSIMAMIA UBORESHAJI ELIMU



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, akifungua Mkutano wa Viongozi wa Maafisa Elimu Kata, Aprili 8, 2021 jijini Dodoma.*

**Na Veronica Simba**

Maafisa Elimu Kata kote nchini wametakiwa kutimiza wajibu wao wa kutoa msaada wa kitaaluma ili kuwawezesha walimu katika maeneo yao kufundisha kwa ufanisi na hivyo kuboresha kiwango cha elimu.

Wito huo umetolewa na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) David Silinde, alipokuwa akifungua Mkutano wa Viongozi wa Maafisa Elimu Kata, Aprili 8 mwaka huu, jijini Dodoma.

Aidha, Naibu Waziri Silinde, amewataka Maafisa Elimu Kata kusimamia kikamilifu ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari huku akieleza kuwa imebainika baadhi ya Maafisa hao hawasimamii shule za sekondari.

"Mnajikita zaidi katika shule za msingi na kujisahau kusimamia shule za sekondari. Kote ni wajibu wenu na hakuna mtu anayepaswa kuwazuia. Akijitokeza wa kuwazuia tupeni taarifa tutamchukulia hatua," alisisitiza.

Akiwasilisha mada kuhusu majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu katika Mkutano huo, Mkurugenzi Msaidizi, Maadili na Nidhamu, Mwalimu Robert Lwikolela aliwataka Maafisa Elimu hao kushughulikia makosa yanayofanywa na walimu, ambayo hayapewi umuhimu kwa kudhaniwa ni madogo.

Akifafanua, Mwl. Lwikolela alitoa mfano wa kosa la utoro kwa walimu kuwa pamoja na kuathiri utoaji elimu lakini limekuwa halitiliwi maanani kwa kuchukuliwa kama halina uzito.

"Wako baadhi ya Walimu hata hawaandai Mpango wa Somo (Lesson Plan) na wanafundisha vipindi vichache tofauti na walivyopangiwa lakini wanaachwa tu. Ni wajibu wenu kuwafuatilia hao na kushirikiana na Wakuu wa Shule katika kuwarudisha kwenye mstari."

Hata hivyo, akitoa ufafanuzi zaidi katika masuala ya nidhamu kwa walimu, Mkurugenzi Msaidizi, Ajira na Maendeleo ya Walimu, Mectildis Kapinga, alisema endapo Mwalimu atabainika kutenda kosa, anayepaswa kutoa adhabu kwake kwa mujibu wa sheria ni Mamlaka yake ya Nidhamu ambayo ni Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), na siyo vinginevyo.

Hivyo aliwatahadharisha Maafisa Elimu Kata kutojichukulia sheria mkononi badala yake, ikitokea wamebaini Mwalimu anakiuka maadili ya kazi yake, washirikiane na Mkuu wa Shule kumkanya ili abadili mwenendo wake na asipojirekebisha wamripoti kwa Mamlaka yake ya Nidhamu ili imchukulie hatua.

Kwa upande wake, akitilia mkazo suala la uwajibishaji walimu wanaokiuka maadili ya kazi, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu kutoka

# MAAFISA ELIMU KATA WAASWA KUSIMAMIA UBORESHAJI ELIMU



*Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweli, akizungumza wakati wa siku ya kwanza ya Mkutano wa Viongozi wa Maafisa Elimu Kata, Aprili 8, 2021 jijini Dodoma.*

TSC, Moses Chitama, alishauri kabla ya mwalimu kuripotiwa kwa Tume, zifanyike jitihada katika ngazi ya shule na kata, kukaa na kuzungumza naye ili kumkanya, hususan kwa makosa madogomadogo ambayo yanarekebishika.

Mkutano huo wa Maafisa Elimu Kata ulihitimishwa rasmi Aprili 9, 2021 ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu.



*Mkurugenzi kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayesimamia Elimu ya Awali na Msingi ambaye pia ni Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Suzan Nussu, akizungumza wakati wa siku ya kwanza ya Mkutano wa Viongozi wa Maafisa Elimu Kata, Aprili 8, 2021 jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama akichangia mada katika siku ya kwanza ya Mkutano wa Viongozi wa Maafisa Elimu Kata, Aprili 8, 2021 jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi Msaidizi, Maadili na Nidhamu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwalimu Robert Lwikolela akiwasilisha mada kuhusu majukumu ya Tume wakati wa siku ya kwanza ya Mkutano wa Viongozi wa Maafisa Elimu Kata, Aprili 8, 2021 jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi Msaidizi, Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mectildis Kapinga akichangia mada wakati wa siku ya kwanza ya Mkutano wa Viongozi wa Maafisa Elimu Kata, Aprili 8, 2021 jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Maafisa Elimu Kata, Wilaya ya Kyerwa, Oscar Tumwesige, akichangia mada wakati wa siku ya kwanza ya Mkutano wa Viongozi wa Maafisa Elimu Kata, Aprili 8, 2021 jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Maafisa Elimu Kata, Wilaya ya Bagamoyo, Hamisi Mwanankuta, akichangia mada wakati wa siku ya kwanza ya Mkutano wa Viongozi wa Maafisa Elimu Kata, Aprili 8, 2021 jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Maafisa Elimu Kata, Wilaya ya Muheza, Danstan Mahiza, akichangia mada wakati wa siku ya kwanza ya Mkutano wa Viongozi wa Maafisa Elimu Kata, Aprili 8, 2021 jijini Dodoma.*



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde (katikati) akiungana na Wajumbe wa Mkutano wa Viongozi wa Maafisa Elimu Kata, kuimba Wimbo wa Taifa, muda mfupi kabla ya kufungua Mkutano huo Aprili 8, 2021 jijini Dodoma. Kulia kwake ni Naibu Katibu Mkuu, TAMISEMI anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweli.*



*Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama (kulia-mbele) na Mkurugenzi Msaidizi, Ajira na Maendeleo ya Walimu Mectildis Kapinga (wa tatu kutoka kushoto – mbele), wakiwa pamoja na viongozi mbalimbali wa Serikali katika siku ya kwanza ya Mkutano wa Viongozi wa Maafisa Elimu Kata, Aprili 8, 2021 jijini Dodoma.*







*Sehemu ya wajumbe wa Mkutano wa Viongozi wa Maafisa Elimu Kata, wakifuatilia mkutano huo katika siku ya kwanza, Aprili 8, 2021 jijini Dodoma.*

# PROF. SHEMDOE AWAONYA MATAPELI KUHUSU AJIRA ELFU SITA ZA WALIMU

**Veronica Simba na Atley Kuni**

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, ametoa onyo kwa watu wanaowatapeli wananchi sehemu mbalimbali kwamba wanahusika kwa namna moja ama nyingine katika zoezi la kuajiri walimu 6,000 ili kujaza nafasi zilizoachwa wazi, kama ilivyoagizwa na Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni.

Alitoa onyo hilo Aprili 23, 2021 mbele ya waandishi wa habari wakati wa ziara yake ya kwanza Makao Makuu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Dodoma, iliyolenga kujionea utekelezaji wa majukumu yao pamoja na kuzungumza na watumishi.

Prof. Shemdoe aliwataka watumishi wa umma kuepuka kujihusisha na utapeli huo kwani wakibainika watachukuliwa hatua kali za kinidhamu na kisheria ikiwemo kufukuzwa kazi. Aidha, kuhusu vishoka wanaojihusisha na utapeli huo, Prof. Shemdoe alisisitiza kuwa TAMISEMI itapambana nao vikali.

"Mtumishi atakayebainika kujiingiza kwenye suala hili la utapeli anaweza kupoteza kazi. Kwa wale vishoka ambao wameamua kujichukulia fedha za watanzania wenzetu wakiwahadaa kuwa watawatafutia ajira, tutapambana nao vikali na tutahakikisha sheria



*Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe (katikati), akizungumza na Wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu – TSC (hawapo pichani), alipotembelea Taasisi hiyo jijini Dodoma Aprili 23, 2021 kujionea utekelezaji wa majukumu. Kushoto kwake ni Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, anayehusika na masuala ya Elimu, Gerald Mweli na kulia kwake ni Katibu wa TSC Mwl. Paulina Nkwama.*



*Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe (mbele-katikati), akizungumza na Wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), alipotembelea Taasisi hiyo jijini Dodoma Aprili 23, 2021 kujionea utekelezaji wa majukumu. Kushoto kwake ni Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, anayehusika na masuala ya Elimu, Gerald Mweli na kulia kwake ni Katibu wa TSC Mwl. Paulina Nkwama.*

# PROF. SHEMDOE AWAONYA MATAPELI KUHUSU AJIRA ELFU SITA ZA WALIMU

inachukua mkondo wake."

Kufuatia hali hiyo, Prof Shemdoe alibainisha kuwa ajira husika zitatolewa kwa kuzingatia vigezo vitakavyoainishwa katika tangazo litakalotolewa na Ofisi yake, na kwamba hakutakuwa na upendeleo wa aina yoyote.

"Hakuna mtu atakayependelewa na hatutaangalia nani katoka wapi. Hizi ni ajira za watanzania wote, hivyo tutaangalia vigezo ambavyo tutaviainisha katika tangazo ambalo tutalitoa kwa wananchi na siyo vinginevyo," alisisitiza.

Aidha, alimwagiza Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, anayehusika na masuala ya Elimu, Gerald Mweli pamoja na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama kukaa pamoja na kuunda timu itakayoshughulikia ajira hizo, huku akisisitiza kuwa timu hiyo iundwe na watu wenye hofu ya Mungu ili watende haki.

Alisema Ofisi yake itaendelea kuomba nafasi zaidi za ajira kwani inatambua kuwa wapo vijana wengi



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akimkaribisha Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe (wa tatu-kushoto) kuzungumza na Wajumbe wa Menejimenti ya Tume hiyo. Prof Shemdoe alitembelea Makao Makuu ya TSC jijini Dodoma, Aprili 23, 2021 kujionea utekelezaji wa majukumu yao. Kushoto kwa Katibu Mkuu ni Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI, anayehusika na masuala ya Elimu, Gerald Mweli.*



*Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, anayehusika na masuala ya Elimu, Gerald Mweli (katikati), akizungumza na watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), wakati wa ziara ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe (wa pili-kushoto), Aprili 23, 2021 Makao Makuu ya Tume Dodoma. Wa kwanza kushoto ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.*



*Baadhi ya wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakimsikiliza Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe (wa pili-kushoto) alipotembelea Makao Makuu ya TSC jijini Dodoma, Aprili 23, 2021 kujionea utekelezaji wa majukumu yao. Kushoto kwa Katibu Mkuu ni Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI, anayehusika na masuala ya Elimu, Gerald Mweli na wa kwanza kushoto ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.*

# PROF. SHEMDOE AWAONYA MATAPELI KUHUSU AJIRA ELFU SITA ZA WALIMU

waliohitimu lakini hawajapata ajira.

Katika hatua nyingine, Katibu Mkuu aliipongeza TSC kwa kazi nzuri inayofanya hususani katika kusimamia maadili kwa walimu walioko katika utumishi wa umma. Aliwataka watendaji wa Taasisi hiyo kuendelea kutimiza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu hasa wakati wa kufanya maamuzi katika mashauri ya walimu yanayofikishwa kwao.

"Serikali imewapa dhamana na imani kubwa katika kusimamia maadili ya walimu. Nawaomba muendelee kufanya kazi hiyo kwa imani ileile ambayo mmepewa."

Prof Shemdoe alimpongeza Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Rais Samia kushika wadhifa huo. Aliwataka watumishi wote kumpa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yake.

Akizungumza katika ziara hiyo, Naibu Katibu Mkuu Mweli, alimweleza Katibu Mkuu kuwa



*Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, akisaini Kitabu cha Wageni, Ofisini kwa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa pili-kulia). Katibu Mkuu alitembelea Makao Makuu ya Tume jijini Dodoma, Aprili 23, 2021. Wa pili kutoka kushoto ni Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, anayehusika na masuala ya Elimu, Gerald Mweli, wa kwanza kushoto ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu TSC, Moses Chitama na wa kwanza kulia ni Mkurugenzi Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu TSC, Christina Hape.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto), akimkaribisha Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe (katikati) na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI, anayehusika na masuala ya Elimu, Gerald Mweli (kulia), walipowasili Makao Makuu ya Tume jijini Dodoma, Aprili 23, 2021 wakiwa katika ziara ya kazi.*

# PROF. SHEMDOE AWAONYA MATAPELI KUHUSU AJIRA ELFU SITA ZA WALIMU

TSC imekuwa ikifanya kazi nzuri ambapo alibainisha kuwa tangu ashike nafasi hiyo, Tume imetekeleza kazi walizokubaliana kwa asilimia 90.

Kwa upande wake, akizungumza kwa niaba ya watumishi wote wa TSC, Katibu wa Tume Mwl. Nkwama alisema kuwa wamefarijika sana kupata heshima ya kuwa miongoni mwa taasisi za mwanzo zilizo chini ya TAMISEMI, kutembelewa na Katibu Mkuu ili kujionea utendaji wao.

"Tumefarijika sana na ujio wako hasa kwa kuzingatia kuwa ni takriban majuma mawili tu tangu ulipoapishwa na Mhe. Rais kushika wadhifa wa Katibu Mkuu TAMISEMI. Kwa kuthamini, mchango wa kada ya walimu, umeona ziara yako ya kwanza ujielekeze kwenye Ofisi ya Tume ambayo ndiyo yenye kushughulikia masuala mbalimbali ya walimu. Tunaskushukuru sana," alisema.

Tume ya Utumishi wa Walimu ndiyo Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa walimu walioko katika utumishi wa umma Tanzania Bara.





*Baadhi ya wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakimsikiliza Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe (hayupo pichani), aliyekuwa akizungumza nao alipotembelea Makao Makuu ya TSC jijini Dodoma, Aprili 23, 2021 kujionea utekelezaji wa majukumu yao.*

# MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WA ZIARA YA KATIBU MKUU OFISI YA RAIS – TAMISEMI, PROF RIZIKI SHEMDOE MAKAO MAKUU YA TSC DODOMA











# KATIBU MPYA TSC AANZA KAZI RASMI

**Veronica Simba na Adili Mhina**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwalimu Paulina Nkwama, ameripoti Ofisini kwake, Makao Makuu ya Tume, jijini Dodoma na kuanza kazi rasmi.

Mwl. Nkwama ameanza majukumu yake, Aprili 1, 2021 baada ya kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kushika wadhifa huo kuanzia Machi 29 mwaka huu, akichukua nafasi ya Winfrida Rutaindurwa ambaye amemaliza muda wake.

Akizungumza na Menejimenti ya TSC, muda mfupi baada ya kuwasili ofisini hapo, Mwl. Nkwama alisisitiza upendo, ushirikiano na mshikamano miongoni mwa watumishi ili kwa pamoja waweze kutimiza azma ya kuihudumia vyema kada wanayoisimamia, yaani Walimu walio katika Utumishi wa Umma.



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (kushoto), akimkaribisha Katibu wa Tume hiyo, Mwl. Paulina Nkwama katika Ofisi yake mpya, Makao Makuu ya Tume, Dodoma, baada ya kuripoti rasmi na kuanza kazi, Aprili 1, 2021.*



*Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama (kulia), akimkabidhi Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, Ripoti kuhusu Tume husika, wakati wa hafla fupi ya kumkaribisha Ofisini kwake, Makao Makuu Dodoma, baada ya kuripoti rasmi na kuanza kazi, Aprili 1, 2021.*

"Kwenye Taasisi kukiwa hakuna upendo ni changamoto, hivyo nawaomba tupendane, tushirikiane na tushikamane. Tukienda hivyo, naamini kwa msaada wa Mungu, tutafanikiwa."

Aidha, Mwl. Nkwama alitumia nafasi hiyo kueleza shukrani zake kwa Mwenyezi Mungu kwa kumwezesha katika hatua mbalimbali za maisha yake hadi kufikia mahali alipo na pia alimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumwamini na kumteua kushika wadhifa husika.

"Naamini Mheshimiwa Rais aliwaona wengi ambao wana sifa za kushika wadhifa huu, lakini akaniamini mimi na kunipa nafasi ya kuwatumikia Watanzania hususani Walimu ambao Tume

# KATIBU MPYA TSC AANZA KAZI RASMI



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, akiendelea na majukumu Ofisini kwake, Makao Makuu Dodoma, muda mfupi baada ya kuripoti rasmi na kuanza kazi, Aprili 1, 2021.*

itaendelea kufanya kazi nzuri.

Akizungumza katika hafla hiyo fupi ya ukaribisho, aliyekuwa Kaimu Katibu wa TSC, Moses Chitama alieleza kuwa Tume imepokea uteuzi wa Mwl. Nkwama kwa furaha kubwa na kwamba wana imani naye.

Akizungumza kwa niaba ya Menejimenti na Wafanyakazi wote, Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu Christina Hape, aliahidi kuwa watampatia ushirikiano Katibu Nkwama ili aweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Awali, akiwasilisha Taarifa fupi kuhusu TSC kwa Katibu huyo, Mkurugenzi Msaidizi wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Shani Kamala, alibainisha jukumu kuu la Tume kuwa ni kuendeleza na kusimamia Utumishi wa Walimu.

Kabla ya uteuzi wake, Mwl. Nkwama alikuwa Katibu Tawala Msaidizi (Elimu), Mkoa wa Kilimanjaro.

hii inawasimamia. Namshukuru sana na ninaahidi sitamwangusha," alieleza Mwl. Nkwama.

Vilevile, aliwataka watumishi wote wa TSC kutambua kuwa yeyé ni mtumishi mwenzao hivyo waache kumwogopa kutokana na wadhifa wake. Badala yake aliwataka wawe huru kushirikiana naye katika kazi huku akiahidi kupokea ushauri kutoka kwa yeyote na kuufanyia kazi ili kupata matokeo chanya.

Kwa upande wake, akimkaribisha Katibu, Mwenyekiti wa TSC, Profesa Willy Komba alimpongeza kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kushika nafasi hiyo.

Aidha, Prof. Komba alimweleza Katibu Nkwama kuwa Menejimenti ya TSC ina Wajumbe mahiri wenye weledi na utendaji mahiri wa kazi, hivyo anaamini kupitia uongozi wake, Tume



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (aliyesimama), akizungumza na Wajumbe wa Menejimenti, Makao Makuu Dodoma, muda mfupi baada ya kuripoti rasmi na kuanza kazi, Aprili 1, 2021. Kulia kwake ni Mwenyekiti wa TSC, Prof Willy Komba na kushoto kwake ni aliyekuwa Kaimu Katibu, Moses Chitama.*










*Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Makao Makuu Dodoma, wakimpokea Katibu wa Tume hiyo, Mwl. Paulina Nkwama, alipowasili kuanza kazi rasmi, Aprili 1, 2021.*



*Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Christina Hape (kushoto), akiwasilisha salamu za ukaribisho kwa niaba ya Menejimenti na Wafanyakazi wote, kwa Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama (kulia), baada ya kuripoti rasmi Makao Makuu Dodoma na kuanza kazi, Aprili 1, 2021.*



*Mkurugenzi Msaidizi wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Shani Kamala, akiwasilisha Taarifa kuhusu Tume kwa Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (hayupo pichani), alipokutana na Menejimenti baada ya kuripoti rasmi Makao Makuu Dodoma na kuanza kazi, Aprili 1, 2021.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto), akimshukuru kwa kumfikisha salama na kuagana na aliyekuwa Dereva wake, Sajenti Martin Mwanandota, baada ya kuripoti rasmi Ofisi yake mpya, Makao Makuu Dodoma, Aprili 1, 2021. Kabla ya uteuzi wake, Mwl. Nkwama alikuwa Katibu Tawala Msaidizi (Elimu), Mkoa wa Kilimanjaro.*

# WALIMU WASHAURIWA KUITUMIA TSC KUTATUA KERO ZAO

**Na Adili Mhina**

Walimu wametakiwa kuzitumia kikamilifu ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kuwasilisha kero na changamoto za kiutumishi wanazokutana nazo katika maeneo ya kazi ili ziweze kupatiwa ufumbuzi kwa haraka na kwa wakati.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Christina Hape wakati wa kikao kazi kilichowahusisha walimu wa shule za msingi na sekondari wa Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro.

Kikao hicho kililenga kutoa elimu kwa walimu juu ya masuala ya ajira, maadili na maendeleo ya utumishi wa walimu, kusikiliza changamoto za walimu pamoja na kupata maoni yao juu ya mambo mbalimbali yanayolenga kuboresha utumishi wa walimu nchini.



*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Christina Hape akitoa hotuba yake kwenye kikao cha Walimu wa shule za msingi na sekondari wa Wilaya ya Same. Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni katika ukumbi wa shule ya sekondari Same na kililenga kuwaelimisha walimu juu ya sheria na taratibu za Utumishi wa Walimu.*



*Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule (kulia) akizungumza na Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Christina Hape kuhusu masuala mbalimbali ya utumishi wa walimu. Mazungumzo hayo yalifanyika ofisini kwa Mkuu wa Wilaya hivi karibuni.*

Hape alieleza kuwa Serikali iliamua kuanzisha TSC kwa lengo la kumsaidia mwalimu kutatua kero mbalimbali na kumfanya aweze kutekeleza majukumu yake ya kufundisha wanafunzi katika mazingira ya amani na utulivu.

"TSC ipo kwasababu

# WALIMU WASHAURIWA KUITUMIA TSC KUTATUA KERO ZAO

walimu mpo, tunafanya kazi kwa kuwa ninyi mpo, sisi ni watumishi wenu na tuna wajibu wa kuhakikisha uwepo wetu unawasaidia ninyi kufanya kazi zenu kwa ufanisi. Tupo kwa ajili ya kufanya walimu wafanye kazi kwa furaha na Amani," alisema.

Alifafanua kuwa wapo baadhi ya viongozi wamegeuka kuwa miungu watu na wamekuwa wakiwanyanyasa walimu pale wanapofika kwenye ofisi zao kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali ambazo zimewekwa kwa mujibu wa sheria.

"kuna baadhi ya viongozi wakimuona tu mwalimu ameingia ofisini kwake, hata kabla ya kumsikiliza anaanza kumfokea na kumkaripia mpaka mwalimu anapoteza ujasiri wa kujieleza. Mwingine anagoma kupitisha barua ya mwalimu makusudi tu ili amkomoe mwalimu, bila kuelewa kuwa kufanya hivyo ni kuvunja sheria," alisema Hape.

Alisisitiza kuwa mwalimu ni mtumishi wa umma kama walivyo watumishi wa kada nyingine, hivyo anastahili kuheshimiwa na kuhudumiwa vizuri sehemu yoyote anapoingia ilimradi hajavunja sheria na taratibu za utumishi wake.

Alieleza kuwa pale ambapo mwalimu amekwenda kwenye ofisi ya umma kwa masuala ya kiutumishi na akaona ametendewa kinyume na utaratibu, asikae kimya, badala yake awasilishe malalamiko kwenye ofisi za TSC ili hatua zichukuliwe kwa haraka na aweze kupatiwa haki yake.

"Mwalimu unapaswa kumheshimu kiongozi wako lakini sio kumuogopa. Miongoni mwa majukumu ya TSC kwa mujibu wa sheria ni kushughulikia malalamiko ya walimu. Hivyo, pale unapotendewa ndivyo sivyo usikae kinyonge, leta malalamiko yako sisi tutawasiliana na Mamlaka inayohusika na utapata haki yako," alisema Hape.

Pamoja na hayo, Mkurugenzi Hape aliwataka walimu wilayani humo kuhakikisha wanazingatia nguzo za maadili ya kazi ya ualimu ambazo ni



*Baadhi ya walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Same wakiwa katika hali ya furaha wakati wa kikao kilichowakutanisha na Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Christina Hape.*



*Baadhi ya walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Same waliohudhuria kikao kazi baina yao na Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Christina Hape, wakiwa katika hali ya utulivu wakati kikao kikiendelea.*

# WALIMU WASHAURIWA KUITUMIA TSC KUTATUA KERO ZAO



pamoja na kumlea mtoto kiakili, kimwili, kiroho na kijamii ili kuandaa Taifa la watu wema, wazalendo na walioelimika.

Aliongeza kuwa walimu wanapaswa kusoma na kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayohusu utumishi wa walimu ili kuhakikisha wanafikia malengo ya Serikali katika kuboresha sekta ya elimu nchini.

Naye Kaimu Katibu wa TSC Wilaya ya Same, John Limu alieleza kuwa hali ya nidhamu kwa walimu wilayani hapo ni nzuri kutokana na elimu inayotolewa mara kwa mara juu ya miiko na maadili ya utendaji wa kazi ya ualimu.

"Ndugu Mkurugenzi, hali ya nidhamu kwa walimu wa Wilaya hii ni nzuri, katika kipindi cha miezi sita ni shauri moja tu la nidhamu lililofunguliwa. Ukiangalia hata kiwango cha ufaulu wa wanafunzi kwa wilaya hii ni kizuri. Hii ni kwasababu walimu wetu wanajitahidi kufanya kazi kwa nidhamu na weledi," alisema.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kaimu Katibu Msaidizi, Wilaya ya Same ina jumla ya walimu 1,966 wanaofundisha shule za serikali. Katika idadi hiyo, walimu 1,150 ni wa shule za msingi na walimu 816 ni wa shule za sekondari.



*Baadhi ya walimu wakichangia mada wakati wa kikao kilichowakutanisha Walimu wa Wilaya ya Same na Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Christina Hape.*

# WALIMU MWANGA WAPONGEZWA KWA KUFANYA KAZI KWA NIDHAMU NA WELEDI



*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Christina Hape akitoa hotuba yake kwenye kikao cha walimu wa shule za msingi na sekondari wa Wilaya ya Mwanga. Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni katika shule ya sekondari Mwanga.*



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mwanga, Catherine Kimaro akitoa taarifa fupi ya utendaji kazi wa Ofisi yake wakati wa kikao cha walimu na Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu kilichofanyika hivi karibuni wilayani Mwanga.*



*Mwakilishi wa Afisa Elimu Wilaya ya Mwanga, Hilda Sindato akitoa salamu wakati wa kikao kilichowakutanisha Walimu wa Wilaya hiyo na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu.*

**Na Adili Mhina**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imewapongeza walimu wa Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro, kwa kuendelea kufanya kazi kwa weledi na nidhamu licha ya changamoto mbalimbali zinazowakabili.

Pongezi hizo zimetolewa hivi karibuni na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Christina Hape alipofanya ziara wilayani hapo kwa lengo la kukutana na kuzungumza na walimu juu ya masuala mbalimbali ya kiutumishi.

Hape alieleza kuwa TSC inatambua changamoto mbalimbali za Wilaya hiyo ikiwemo upungufu wa walimu pamoja na shule nyingi kuwa maeneo ya mbali ambapo miundombinu na huduma mbalimbali bado hazijafika.

Aliongeza kuwa, licha ya changamoto hizo, walimu wa Wilaya hiyo wamekuwa mfano wa kuigwa kutokana na moyo wa kufanya kazi kwa bidii na

> **"Hii imefanya hata katika masuala ya kupandisha madaraja sijasikia malalamiko kuwa kuna mwalimu amesahaulika."**

# WALIMU MWANGA WAPONGEZWA KWA KUFANYA KAZI KWA NIDHAMU NA WELEDI



*Baadhi ya walimu wa Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro wakisikiliza hotuba ya Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape (hayupo pichani), alipokutana nao hivi karibuni.*

kwa nidhamu, kitu kinachofanya Mkoa wa Kilimanjaro kuendelea kuwa miongoni mwa mikoa inayofanya vizuri kitaaluma.

"Kwa kweli Mwanga mnajitahidi kufanya vizuri, tunatambua kuwa yapo maeneo ya milimani ambayo hata kufikika kwake ni changamoto. Nimeelezwa kuwa hata kufika hapa kwenye mkutano huu wapo baadhi yenu mliolala kwenye magari ili muweze kuwahi," alisema Hape.

Aliongeza kuwa, "pamoja na changamoto hizo mmeendelea kufanya kazi kwa kujituma na kwakweli hata kule Makao Makuu hatujapokea rufaa nyingi zinazohusu utovu wa nidhamu kwa walimu wa Mwanga, naomba niwapongeze sana kwa hilo."

Mkurugenzi Hape alifafanua kuwa, suala la upungufu wa walimu siyo la Wilaya hiyo peke yake bali maeneo mengi ya nchi kuna upungufu wa walimu na tayari Serikali imeamua kuchukua hatua za haraka ili kukabiliana na tatizo hilo.

"Mtakumbuka kuwa hivi karibuni Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alizungumzia suala la upungufu wa walimu na kuagiza



*Baadhi ya walimu na wathibiti ubora wa shule wa Wilaya ya Mwanga wakifuatilia hotuba ya Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape (hayupo pichani).*

# WALIMU MWANGA WAPONGEZWA KWA KUFANYA KAZI KWA NIDHAMU NA WELEDI



*Mmoja wa walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga akiuliza swali wakati wa kikao cha Walimu na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape (hayupo pichani), kilichofanyika hivi karibuni.*

suala hilo tulishughulikie kwa haraka. Vilevile, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu naye amesisitiza kuwa hataki kuona shule yenye walimu wawili au watatu," alisema Hape.

Aliongeza kuwa maagizo ya viongozi hao kuhusu kutatua changamoto ya upungufu wa walimu inaifanya TSC pamoja na mamlaka nyingine zinazohusika kuchukua hatua za haraka kuhakikisha walimu wanaajiriwa ili kujaza maeneo yenye upungufu.

Pamoja na hayo, Mkurugenzi huyo alipongeza ushirikiano uliopo kati ya Ofisi ya TSC Wilaya pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga na kusema kuwa ushirikiano huo ndiyo unaofanya walimu wafanye kazi kwa moyo, nidhamu na weledi.

"Nishukuru Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji pamoja na Ofisi ya TSC Wilaya kwa kuwa mnafanya kazi kama timu moja, hakuna mivutano. Kaimu Katibu wa TSC, Maafisa Elimu pamoja na Maafisa Utumishi mnazungumza lugha moja katika kutatua kero za walimu. Hii imefanya hata katika masuala ya kupandisha madaraja sijasikia malalamiko kuwa kuna mwalimu amesahaulika," alisema Hape.

Akitoa taarifa fupi ya utendaji wa TSC wilayani hapo, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mwanga, Catherine Kimaro alisema kuwa, Wilaya hiyo ina jumla ya walimu 1,120 wanaofundisha shule za Serikali. Katika idadi hiyo, walimu 558 ni wa shule za msingi na 562 ni wa shule za sekondari.

Kimaro alieleza kuwa, Wilaya hiyo kwa sasa haina shauri lolote la nidhamu kutokana na juhudi za Ofisi yake za kutoa elimu kwa walimu mara kwa mara kuhusu miiko na maadili ya utendaji wa kazi.



*Mmoja wa walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga akitoa maoni ya masuala ya utumishi wa walimu wakati wa kikao cha Walimu na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape (hayupo pichani), kilichofanyika hivi karibuni.*

# WALIMU KILOLO WAONYWA UHUSIANO WA MAPENZI NA WANAFUNZI

**Na Adili Mhina**

Walimu wilayani Kilolo, Mkoa wa Iringa wametakiwa kuacha mara moja tabia ya kujihusisha kimapenzi na wanafunzi kwani kufanya hivyo ni kukiuka maadili, kudhalilisha kazi ya ualimu, kuhatarisha ajira na kukatisha ndoto za wanafunzi.



*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Christina Hape akitoa hotuba yake kwenye Mkutano wa walimu wa Wilaya ya Kilolo uliofanyika katika ukumbi wa Shule ya Sekondari Kilolo, hivi karibuni. Kushoto ni Afisa Elimu Msingi wa Wilaya ya Kilolo, Alloys Maira na kulia ni Afisa Mwandamizi kutoka TSC Makao Makuu, Neema Lemunge.*



*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Christina Hape (kushoto) akimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Laini Kamendu juu ya hali ya nidhamu ya walimu katika Wilaya hiyo. Mazungumzo hayo yalifanyika katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Kilolo hivi karibuni.*

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Christina Hape alipofanya mkutano na walimu wa Wilaya hiyo kwa lengo la kutoa elimu juu ya sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa walimu.

Katika Mkutano huo uliofanyika kwenye ukumbi wa Shule ya Sekondari Kilolo iliyopo wilayani hapo, Hape alieleza kuwa Kilolo ni moja ya Wilaya zenye idadi kubwa ya mashauri ya nidhamu yanayohusu walimu kuwa na uhusiano wa mapenzi na wanafunzi, jambo ambalo linadhalilisha kazi ya ualimu.

"Kilolo kuna tatizo kubwa la walimu kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi, wote tunatambua kuwa hii ni kuvunja miiko na maadili ya ualimu. Wazazi wametukabidhi watoto ili tuwalee kimwili, kiroho na kiakili lakini baadhi yetu wamewafanya wanafunzi kuwa

# WALIMU KILOLO WAONYWA UHUSIANO WA MAPENZI NA WANAFUNZI

wapenzi wao, jambo hili halivumiliki," alisema Hape.

Aliongeza kuwa, kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo, wazazi na jamii kwa ujumla inaanza kukosa imani na walimu juu ya usalama wa watoto wao wawapo shuleni, kitu ambacho kinarudisha nyuma maendeleo ya sekta ya elimu nchini.

Alisisitiza kuwa, moja ya njia za kutokomeza tatizo hilo ni kuhakikisha kila mwalimu anakuwa mlinzi wa mwenzake ili pale inapotokea kuna mmoja anajihusisha na vitendo hivyo, taarifa itolewe mara moja na hatua stahiki zichukuliwe kwa haraka.

"Ni lazima sasa kila mmoja wetu ajitahidi kulinda hadhi na heshima ya mwalimu, tusikubali kudharaulika kwa sababu ya watu wachache. Kila mwalimu awe mlinzi kwa mwenzake, ukiona kuna mwenzako anafanya vitendo hivyo, toa taarifa kwa Mkuu wa Shule, kama hachukui hatua nenda ngazi inayofuata hadi pale hatua zitakapochukuliwa," alisema Hape.



*Mwalimu Daniel Kamwela wa shule ya msingi Ndengisivili iliyopo Halmashauri ya wilaya ya Kilolo, akiuliza swali wakati wa Mkutano uliowakutanisha walimu wa Wilaya ya Kilolo na Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Christina Hape (hayupo pichani) kutoka TSC Makao Makuu.*



*Mwalimu Clementina Kilumile wa shule ya msingi Pomerini iliyopo Halmashauri ya wilaya ya Kilolo, akiuliza swali wakati wa Mkutano uliowakutanisha walimu wa Wilaya ya Kilolo na Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Christina Hape (hayupo pichani) kutoka TSC Makao Makuu.*

Aliongeza kuwa TSC haipo kwa ajili ya kuwafukuza kazi walimu, ndiyo maana wakati wote imekuwa mstari wa mbele kuwaelimisha walimu juu ya kanuni na taratibu za utumishi wao ili wasijiingize kwenye makosa ya kinidhamu yanayoweza kukatisha ajira zao.

"TSC tunawapenda sana walimu, hatupendi hata mwalimu mmoja apoteze ajira yake. Wote tunajua kuwa walimu waliopo bado ni wachache, tukiwafukuza tatizo la upungufu wa walimu linaongezeka, lakini pamoja na hayo, hatuwezi kuwafumbia macho walimu ambao hawataki kubadilika, hao lazima tuwaondoe," alisema.

Kabla ya kufanya mkutano na walimu, Mkurugenzi Hape alifanya mazungumzo mafupi na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Laini Kamendu ambaye alikiri kukithiri kwa tatizo hilo kwenye halmashauri yake.

Kamendu alieleza

# WALIMU KILOLO WAONYWA UHUSIANO WA MAPENZI NA WANAFUNZI

kuwa tatizo hilo kwa kiasi kikubwa lipo maeneo ya vijijini ambapo wananchi bado hawajawa na mwamko mkubwa katika kuwalinda watoto dhidi ya vitendo visivyofaa ikiwemo vya walimu kuwa na uhusiano wa mapenzi na wanafunzi.

Aliongeza kuwa kutokana na ugumu wa maisha ya vijijini, baadhi ya walimu wasiozingatia maadili ya kazi yao wanatumia mwanya huo kuwarubuni wanafunzi kwa vitu vidogo vidogo na hatimaye wanawageuza kuwa wapenzi wao.

"Watoto wengi wanaofanyiwa vitendo hivyo wapo maeneo ya vijijini, kwa mfano, kuna eneo linaitwa Itonya, huko hata Pikipiki kufika ni shida. Wanafunzi kule hawana uelewa wa mambo mengi kutokana na mazingira, kule mwalimu anaonekana ndiyo kila kitu, chochote atakachotaka mwanafunzi atakubali na matokeo yake ndoto zao zinazimwa," alisema Kamendu.

Alieleza kuwa ofisi yake imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuwasilisha taarifa za walimu wenye uhusiano wa mapenzi na wanafunzi kwenye ofisi za TSC wilayani hapo ili hatua za kinidhamu zichukuliwe kama sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu ya mwaka 2015 inavyoelekeza.

Hata hivyo, Mkurugenzi huyo alishauri TSC kutoa mapendekezo kwa Waziri mwenye dhamana ili ikiwezekana afanye marekebisho ya kanuni za sheria hiyo ili kutotoa mwanya wa kuwaachia huru walimu wanaofanya vitendo vya mapenzi na wanafunzi kwa kisingizio cha kukosa ushahidi wa moja kwa moja.

"Kwa kweli kwa hatua tulizochukua, tatizo la walimu kujihusha na mapenzi na wanafunzi limepungua sana. Kinachonisikitisha ni kwamba TSC ngazi ya Wilaya inawafukuza kazi walimu hawa lakini wanapokata rufaa makao makuu wanashinda na wanarudishwa kazini.





*Baadhi ya walimu wakiwa katika hali ya utulivu wakati wa hotuba ya Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC Makao Makuu, Christina Hape (hayupo pichani).*

Tunaambiwa eti hakuna ushahidi wa kutosha, lakini huko mtaani kila mtu anajua hao walimu ni tatizo kwa wanafunzi. Ni vyema muangalie upya kanuni hizo ili tuwasaidie watoto," alisisitiza Kamendu.

Hape alimweleza Kamendu kuwa TSC imeona changamoto hiyo na ipo kwenye utaratibu wa kutoa mapendekezo ya kumshauri Waziri mwenye dhamana ili kufanya maboresho ya kanuni hizo na kuziba mianya inayowawezesha watuhumiwa kuwarubuni mashahidi ili wasipatikane na hatia.

# ZIARA YA TSC MASHULENI YALETA MATOKEO CHANYA TUNDURU



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Tunduru, Julius Nchimbi (wa nne kutoka kushoto mstari wa pili), akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya walimu wa Kata ya Mbati wilayani Tunduru. Nchimbi alikuwa katika ziara ya kazi hivi karibuni.*

**Fikiri Malibiche na Festo Msagamasi**

Imeelezwa kuwa, ziara za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Tunduru katika Shule mbalimbali, zenye lengo la kuelimisha walimu kuhusu maadili na nidhamu kazini, zimeleta matokeo chanya.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC, Wilaya ya Tunduru, Julius Nchimbi alipokuwa akiwasilisha taarifa ya utendaji kazi wa ofisi yake kwa Ujumbe wa TSC Makao Makuu, uliotembelea ofisi hiyo hivi karibuni kujionea utekelezaji wa majukumu pamoja na kuzungumza na watumishi.

Akieleza zaidi, Nchimbi alisema kuwa ziara hizo zimewezesha walimu kupata elimu mtambuka ikiwemo kujua maadili ya kazi ya ualimu, makosa na adhabu wanazopaswa kuchukuliwa wanapotenda makosa hayo.

"Walimu wengi wamepata elimu hiyo kwa undani, shule hadi shule na kwakweli katika kipindi cha mwezi Oktoba hadi Disemba, Ofisi yetu haikupokea tuhuma zozote zinazohusu ukiukwaji wa maadili kwa walimu kutoka kwa Waajiri."

Akizungumza na watumishi wa Ofisi hiyo, Afisa wa TSC kutoka Makao Makuu, anayeshughulikia Utumishi na Ajira, Francis Gwankisa aliwataka kuendeleza utamaduni wa kutoka ofisini na kwenda shuleni kutoa elimu kwa walimu.

"Inashangaza kuona baadhi ya Ofisi zetu za Wilaya ambazo hazijawahi kutoka kwenda kufanya ziara mashuleni eti kwa kukosa fedha! Ukiwauliza kama walishawahi kuomba fedha hizo za kufanya ziara, hawana majibu! Hatuwezi kujua mahitaji yenu pasipo ninyi kuomba," alisisitiza Gwankisa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi, Ajira na Maendeleo ya Walimu, Mectildis Kapinga aliwataka Kaimu Makatibu wa TSC ngazi ya Wilaya kuwa na Mpango Kazi.

Akifafanua, alisema Mpango Kazi ni dira ya utendaji kazi inayobainisha namna ya utekelezaji hivyo akawataka kutekeleza agizo hilo mara moja.

Aidha, Kapinga aliwataka kuzingatia kuandaa taarifa za utendaji kazi wa Ofisi zao kwa kuzingatia

# ZIARA YA TSC MASHULENI YALETA MATOKEO CHANYA TUNDURU




*Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Makao Makuu, Mectildis Kapinga, akitoa neno fupi kwa watumishi wa Idara za Elimu Msingi, Elimu sekondari, Wathibiti Ubora wa shule pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Tunduru. Pembeni yake ni Afisa Utumishi kutoka TSC Makao Makuu, Francis Gwankisa. Ujumbe wa TSC Makao Makuu ulikuwa katika ziara ya kazi hivi karibuni.*

Mwongozo maalumu waliopatiwa kutoka Makao Makuu ambao unamtaka mtoa taarifa kujumuisha takwimu na majina ya wahusika katika kila tukio analolitolea taarifa.

Katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2021, Ofisi ya TSC, Wilaya ya Tunduru imefanya ziara katika shule 32 ambapo kati yake, saba (7) ni za sekondari na 25 ni za msingi.

Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Machi 2021, Ofisi hiyo imefanikiwa kufanya ziara katika shule 18, zikiwemo mbili (2) za sekondari na 16 za msingi.

Kwa mujibu wa Kaimu Katibu Msaidizi Nchimbi, Ofisi yake inaendelea na zoezi la kutembelea shule zilizosalia katika Wilaya hiyo. Lengo ni kuzifikia zote kulingana na Mpango Kazi uliopo.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Tunduru, Julius Nchimbi akitoa neno mbele ya Maafisa wa Tume Makao Makuu na Maafisa Idara za Elimu Msingi, Elimu Sekondari na Wathibiti Ubora wa Shule wa Wilaya ya Tunduru. Ujumbe wa TSC Makao Makuu ulikuwa katika ziara ya kazi kujionea utekelezaji wa majukumu katika Wilaya hiyo.*

# TSC QUEENS BINGWA BONANZA LA MEI MOSI

**Na Veronica Simba**

Timu ya Mpira wa Pete kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC Queens), imetwaa ushindi wa kwanza katika bonanza maalum la michezo kwa Taasisi za Serikali, lililofanyika Aprili 24 mwaka huu, jijini Dodoma.

**"TSC tunathamini michezo kwani tunaamini ina mchango mkubwa katika kujenga afya za watumishi wetu. Ndiyo maana sisi kama viongozi tumeweka mikakati ya kuhakikisha watumishi wanafanya mazoezi mara kwa mara na kushiriki katika michezo mbalimbali."**

TSC Queens ilitwaa ushindi huo baada ya kuwabwaga washindani wao kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa waliochuana nao vikali katika ngazi ya fainali kwa magoli 25 kwa moja.



*Wachezaji wa Timu ya Mpira wa Pete kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC Queens) wakiwa katika pozi la ushindi baada ya kuichakaza Timu kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa kwa mabao 25 kwa 1, katika fainali za Bonanza la Michezo ya Mei Mosi lililoshirikisha Taasisi mbalimbali za Serikali, Mkoa wa Dodoma, Aprili 24, 2021.*

Awali, Timu hiyo machachari ilipambana na Timu kutoka Wizara ya Fedha na kufanikiwa kuwachakaza mabao 29 kwa 5, hatua iliyowawezesha kufuzu kuingia ngazi ya fainali.

Akizungumzia siri ya ushindi huo wa kishindo, Mlezi wa TSC Queens ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimaliwatu, Shani Kamala alisema ni kutokana na kujituma katika kufanya mazoezi ya mara kwa mara.

"TSC tunathamini michezo kwani tunaamini ina mchango mkubwa katika kujenga afya za watumishi wetu. Ndiyo maana sisi kama viongozi tumeweka mikakati ya kuhakikisha watumishi wanafanya mazoezi mara kwa mara na kushiriki katika michezo mbalimbali," alifafanua.

# TSC QUEENS BINGWA BONANZA LA MEI MOSI




*Dafroza Luhwoga ambaye ni mchezaji wa Timu ya Mpira wa Pete kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC Queens), akifunga goli wakati wa mchezo wa fainali baina ya timu hiyo na wapinzani wao kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa. TSC Queens ilishinda kwa mabao 25 kwa 1. Mashindano hayo yalifanyika Aprili 24 wakati wa Bonanza la Michezo lililoshirikisha Taasisi mbalimbali za Serikali Mkoa wa Dodoma.*

Wakati huohuo, Timu ya Mpira wa Miguu kutoka TSC (TSC Sports Club) waliibuka washindi wa tatu baada ya kuwachabanga mikwaju 5 ya Penalti wapinzani wao ngazi ya nusu fainali, Timu kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa ambao waliambulia mikwaju 2 tu.

Kwa upande wake, Kapteni wa TSC Sports Club, Bitwalihat Magota amesema kikosi chake Kiko vizuri isipokuwa wanahitaji kuongeza zaidi mazoezi na mbinu za kimchezo.

Bonanza hilo liliandaliwa na Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE), Mkoa wa Dodoma ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Sikukuu ya Wafanyakazi Duniani maarufu kama Mei Mosi, ambayo huadhimishwa tarehe moja ya kila mwezi Mei.



*Kikosi cha Mpira wa Miguu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC Sports Club), kikiwa uwanjani muda mfupi kabla ya kuchuana na Timu kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa katika Bonanza la Michezo ya Mei Mosi lililoshirikisha Taasisi mbalimbali za Serikali Mkoa wa Dodoma, Aprili 24, 2021.*

# TSC QUEENS BINGWA BONANZA LA MEI MOSI



*Wachezaji wa Timu ya Mpira wa Pete kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC Queens) wakiwa na nyuso za furaha baada ya kuichakaza Timu kutoka Wizara ya Fedha kwa mabao 29 kwa 5, katika Bonanza la Michezo ya Mei Mosi lililoshirikisha Taasisi mbalimbali za Serikali, Mkoa wa Dodoma, Aprili 24, 2021.*



*Wafanyakazi kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakishangilia baada ya Timu yake ya Mpira wa Miguu (TSC Sports Club) kuichakaza timu kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa kwa mikwaju 5 ya penati dhidi ya 2 katika Bonanza la Michezo ya Mei Mosi lililoshirikisha Taasisi mbalimbali za Serikali Mkoa wa Dodoma, Aprili 24, 2021.*



*Wachezaji wa Timu ya Mpira wa Miguu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC Sports Club), wakimsikiliza Kapteni wao Bitwalihat Magota (kushoto) akiwapatia maelekezo kabla ya kuchuana na Timu kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa katika Bonanza la Michezo ya Mei Mosi lililoshirikisha Taasisi mbalimbali za Serikali, Mkoa wa Dodoma, Aprili 24, 2021.*

# TSC QUEENS BINGWA BONANZA LA MEI MOSI







*Matukio mbalimbali wakati Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliposhiriki Bonanza la Michezo ya Mei Mosi lililoshirikisha Taasisi mbalimbali za Serikali, Mkoa wa Dodoma, Aprili 24, 2021.*

# TSC QUEENS BINGWA BONANZA LA MEI MOSI










*Matukio mbalimbali wakati Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliposhiriki Bonanza la Michezo ya Mei Mosi lililoshirikisha Taasisi mbalimbali za Serikali, Mkoa wa Dodoma, Aprili 24, 2021.*




**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz* **Tovuti:** *www.tsc.go.tz*

***Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania*** ***tumeyautumishiwawalimutanzania***